

2018

JAHAZI



BARAZA LA KISWAHILI LA ZANZIBAR (BAKIZA)

JARIDA MAALUMU LA KONGAMANO LA PILI LA KISWAHILI LA KIMATAIFA, 2018

MHARIRI MKUU
Muhammed Seif Khatib

WAHARIRI WASAIDIZI
Hamad Khamis Juma
Kijakazi Omar Makame

TATHMINI YA TAFSIRI ZA MATINI ZENYE ASILI YA KIGENI KATIKA GAZETI LA TAIFA LEO NCHINI KENYA

Sarah Ndanu M. Ngesu & Miriam Kenyan Osore

Ikisiri

Lengo la makala hii ni kubainisha, kuchanganua na kutathmini vipengele vya matini vilivyootafsiriwa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili katika gazeti la Taifa Leo nchini Kenya. Katika nchi ya Kenya, waandishi wa habari katika gazeti la kipekee la Kiswahili, Taifa Leo hulazimika kutafsiri matini zenye asili ya kigeni kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Hivyo, waandishi wa gazeti la Taifa Leo hujikuta katika hali ya kuchukua majukumu mawili, kuandika habari na kutafsiri. Matini za kigeni husheheni dhana za kiteknolojia, kimazingira na kiutamaduni ambapo umakinifu na ujuzi wa mfasiri huhitajika. Matini za kigeni tulizochunguza ni zile zinazohusu habari kutoka nje ya Afrika ambazo huandikwa kwa Kiingereza na wanahabari huzitafsiri kwenda Kiswahili. Magazeti ni vyombo vya habari vinavyokidhi mahitaji ya mawasiliano katika jamii. Ni njia mojawapo ya kuwafahamisha wanajamii kuhusu matukio mbalimbali ya kila siku pamoja na kutoa taarifa zilizo mpya kwa haraka na katika maeneo mapana. Aidha, magazeti yana jukumu la kuendeleza lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa. Isitoshe, magazeti yana dhima kuu ya kueneza na kuimarisha istilahi za Kiswahili. Istilahi nyingi za Kiswahili zinazofahamika na kutumiwa ni zile zilizoenezwa kupitia vyombo vya habari kama vile magazeti. Mchakato wa kutafsiri unaofaa unahitaji uchanganuzi sahihi wa muktadha, vipengele vya mtindo na uundaji wa maneno. Matatizo mengi katika lugha ya kimagazeti yanayotokana na changamoto za kutafsiri, utohozi wa msamiati wa kigeni, uundaji wa msamiati usio sanifu na matumizi ya sarufi yasiyofaa. Matokeo ya makala hii yanaonesha kwamba tafsiri za matini zenye asili ya kigeni kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili yanadhihirisha tafsiri tenge. Hata hivyo, habari kwenye matini hizo huwa muhimu. Kuna haja ya kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa katika makala hii ili kufanikisha tafsiri hizo.

1.1 Utangulizi

Nchini Kenya kuna magazeti kadhaa yanayochapishwa katika Kiingereza na moja katika lugha ya Kiswahili. Magazeti haya yote huchapishwa katika Jiji la Nairobi, yote kwa ujumla huwa na makala karibu 400,000. Kwa kulinganisha na mataifa mengine, uandishi wa habari nchini Kenya si wa muda mrefu (Kandagor, 2012). Gazeti la Taifa Leo ndilo gazeti la pekee la Kiswahili nchini Kenya ambalo huchapishwa kila siku na Shirika la Usambazaji Habari la *Nation (Nation Media Group - NMG)*. Gazeti hili lilizinduliwa mapema mnamo mwaka wa 1958 na Charles Hayes, aliyekuwa afisa wa utawala wa kikoloni akishirikiana na mwenzake Tebbutt. Wakati huo lilijulikana kama Taifa na lilikuwa likichapishwa kila wiki, Loughran (2010). Gazeti la Taifa lilikuwa jipya na lenye matumaini makubwa katika soko la wakati huo. Sera yake ilikuwa kuunga mkono mapambano ya Wakenya kujipatia uhuru. Kichwa cha habari cha gazeti la kwanza kilikuwa “*When shall we see freedom.*” Habari hii iliwavutia wananchi wengi wa Kenya waliokuwa na hamu ya kuwa huru. Jina lililopewa gazeti hilo (*Taifa*) kwa Kiingereza “*Nation*” lilifaa sana kwa gazeti hili kwa wakati ambapo waafrika walikuwa makini katika kujipatia jamii huru (Loughran, 2010). Baadhi ya matini katika gazeti hili huandikwa moja kwa moja katika Kiswahili. Hata hivyo, matini nyingine huwa na habari za kigeni ambazo hutafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza katika *Daily Nation*.

Mchakato wa kutafsiri kutoka matini chanzi (MC) ambayo ni ya Kiingereza kwenda matini lengwa (ML), yaani ya Kiswahili husababisha kuhifadhiwa kwa vipengele vingi vya kimuundo na vya kiutamaduni ambavyo huonekana kama vigeni kwa wasomaji wa lugha ya Kiswahili.

2.1 Malengo

Lengo la makala hii ni kuchunguza tafsiri ya vipengele vya matini chanzi (Kiingereza) zenye asili ya kigeni katika gazeti la Taifa Leo nchini Kenya.